BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Saba – Tarehe 17 Septemba, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Taarifa ya Serikali Kuhusiana na Hali ya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusumamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2025.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

30. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi uliopo Wete Pemba kwa miaka mingi huko nyuma ulikuwa ukitumika kwa vikao vya Baraza na Bajeti pamoja na sheria nyingi za nchi hii zimeshawahi kupitishwa katika ukumbi huo. Hata hivyo, hivi sasa vikao vya Baraza havifanyiki na badala yake, ukumbi huo unatumika kwa shughuli nyengine za kiserikali. Sambamba na hilo, wakati Unguja kuna mpango wa kuimarisha shughuli za Baraza kwa kujengwa ukumbi mwengine ikiwemo makaazi ya Wajumbe, upande wa Pemba ambako shughuli za Kamati zinafanyika hali haipo hivyo.

(a) Je, ni ipi hatma ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi wa Wete Pemba katika mpango mzima wa kuboresha utendaji kazi wa Wajumbe kwa Unguja na Pemba.

(b) Kwa kuwa Wajumbe wa Baraza wanaotoka Unguja kwenda Pemba kufanyakazi za Kamati wanakosa makaazi maalumu, kwanini kusiwepo mpango wa kujenga hosteli maalumu za Wajumbe na wafanyakazi wanaotoka Unguja kama wanavyofanya taasisi nyengine kama Bandari, ZSTC na nyengine.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kutafuta eneo jengine lenye nafasi ya kutosha na kujenga ukumbi mwengine na Ofisi za Baraza la Wawakilishi kisiwani Pemba.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

119. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Serikali kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 3 ya mwaka 2015 na Kanuni za Kuzuia Mifuko ya Plastiki za mwaka 2018 zimefanikiwa kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki hapa Zanzibar.

Je, ni sababu zipi zinazopelekea Serikali kushindwa kupiga marufuku matumizi ya pempasi na hasa ikizingatiwa kuwa ni miongoni mwa vitu vinavyochafua mazingiria kwa asilimia kubwa.

195. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Tanzania imeridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD) ambao utekelezaji wake pia unaihusisha Zanzibar.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashiriki kwa utaratibu gani katika kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mkataba huo.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

240. MHESHIMIWA MOHAMMED MANZI HAJI (Jimbo la Mwanakerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kukosekana kwa Kituo cha gari za abiria katika Soko la Mwanakwerekwe, kunapelekea, pamoja na sababu nyengine, msongamano mkubwa wa gari unaosababisha usumbufu mkubwa kwa wafanyabiashara na wananchi wanaofuata huduma mbalimbali katika soko hilo.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha gari za abiria cha kisasa katika eneo hilo la Soko la Mwanakwerekwe.

(b) Kuna utaratibu gani wa muda wa kuweka gari za abiria na za wananchi wanaofuata huduma katika Soko la Mwanakwerekwe, ili kuondoa msongamano wa magari katika barabara kuu ya Soko la Mwanakwerekwe.

<u>Wizara ya Fedha na Mipango:</u>

25. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Hivi karibuni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alinukuliwa na vyombo vya habari akisema kuwa, kutegemea mapato kwa kuweka faini ni mambo ya kikoloni na unyang'anyi. Kauli hiyo inaakisi baadhi ya Taasisi zetu hapa ndani, kuweka viwango vya faini vikubwa ambavyo haviendani na uhalisia wa vipato vya wananchi, kama vile kuweka faini kwa kiwango cha shilingi laki tatu (300,000) ambazo ni sawa na kima cha chini cha mshahara wa mtu.

(a) Je, Serikali imeweka sera au muongozo upi maalumu wa namna ya kuweka viwango vya faini, ili visionekane kuwakomoa wananchi.

(b) Kwa nini utaratibu wa Taasisi zetu wa kutegemea faini kama vyanzo vya mapato usionekane kuwa umepitwa na wakati na kama alivyosema Waziri Mkuu kuwa ni wa kikoloni na unyang'anyi.

(c) Je, ni lini Taasisi zetu zitakaa na kubuni vyanzo vyengine vya mapato badala ya kutegemea mapato kwa kuweka viwango vikubwa vya faini.

301. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Baadhi ya wananchi wanakabiliwa na changamoto za gharama na ucheleweshaji katika kupata namba za usajili wa vyombo vyao.

(a) Je, ni sababu gani zinazosababisha kuchelewa kwa upatikanaji wa namba za usajili wa vyombo.

(b) Ni gharama gani rasmi ambazo mwananchi anatakiwa kulipa kuanzia usajili hadi kupata namba ya usajili wa chombo.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kurahisisha na kuharakisha utoaji wa namba za usajili na kuondoa gharama zisizo za lazima.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

178. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kwa kuwa bahari ni chanzo muhimu cha kujiajiri kwa wananchi wengi wa Zanzibar, na kwa kuwa vijana wengi huzitumia fukwe zetu kwa kufanyia mazoezi na hata kuogelea. Na kwa kuwa kuna Mwekezaji karibu na pwani ya Kama, mkabala na hoteli ya *Sunset Paradise Limited,* amejenga ukuta na kuweka zuio kwa vijana wazawa na wananchi kutolitumia eneo hilo.

(a) Je, Serikali imelifuatilia na kulitambua vipi tatizo hilo.

(b) Kwa nini Serikali haioni kwamba zuio hilo linawanyima uhuru na haki wananachi wake, ya kuyatumia maeneo ambayo ndio rasilimali zao za asili.

(c) Kwanini Serikali na Wawekezaji wasingeimarisha usalama katika mali za Mwekezaji iwapo zuio hilo limewekwa kwa sababu ya kiusalama.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

77. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Mwakilishi Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Hivi karibuni tumeshuhudia na kumuona Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar, akiyatangaza maeneo mbalimbali kama vile Jambiani, Bwejuu, Mzuri, Nungwi, Tumbatu, Shengejuu, Kiuyu, Kambini, Kangagani, Ole, Uwandani, Mabonde ya Kwa Pweza na maeneo mengine, kuwa ni maeneo ya Ardhi ya Akiba ya Serikali. Jambo ambalo limepelekea hofu kwa wananchi, wakifikia kwamba ni mtindo mpya unaotumika wa kuendelea kuwanyang'anya ardhi zao.

Je, Serikali imewashirikisha wananchi wa maeneo hayo kwa kiasi gani.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

17. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Wakaazi wa Mji Mkongwe wamehamishiwa *parking* za kulaza gari zao, kutoka sehemu walizokuwa wakiegesha Darajani na kuhamishiwa katika Maegesho ya Malindi (Malindi Parkings). Sehemu hiyo imekua na changamoto ya masafa marefu lakini pia changamoto ya usalama, pindi wakaazi wanaporejea usiku mkubwa na kuwalazimu kutembea masafa marefu kuweka gari na kurejea majumbani.

(a) Je, lini Mamlaka itawatafutia wakaazi wa Mji Mkongwe *parking* za ziada za kulaza gari zao wakati wa usiku.

(b) Je, lini Mamlaka itawapatia wakaazi wa Mji Mkongwe kadi na bei maalumu kwa ajili ya kulaza gari katika *parking* ya Malindi.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

15. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Ujenzi wa Jengo la Abiria (Terminal 2) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA), ni mradi unaoonekana kujengwa bila ya kufuata taratibu za masharti ya Sheria ya Ununuzi wa Umma.

(a) Ni Mkandarasi gani aliyepewa kazi ya ujenzi wa jengo hilo na kwa gharama za kiasi gani.

(b) Ni ipi tathimini ya ujenzi wa Jengo la Abiria (Terminal 2) na Serikali imeridhika vipi katika ujenzi unaoendelea.

35. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Hivi karibuni Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar, ilitoa tangazo kwa madereva pamoja na watumiaji wengine wa barabara, la kuweka faini kwa makosa mbalimbali ya barabarani. Pamoja na nia nzuri ya kudhibiti matumizi salama ya barabara, bado viwango vya faini vilivyowekwa ni vikubwa mno kulinganisha na hali za maisha na vipato vya wananchi wetu na changamoto ya miundombinu na mipango miji ya nchi yetu.

(a) Je, Sheria gani au Kanuni gani zilizotumika kuweka viwango hivyo vikubwa vya faini kwa wananchi.

(b) Je, kama kuna Kanuni zimeweka viwango hivyo, je kwa kiasi gani Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ya Baraza la Wawakilishi, imepata nafasi ya kuvipitia viwango hivyo.

(c) Je, uwekaji wa faini hizo umezingatia vipi hali ya miundombinu yetu na mipango miji, hasa kwa kuwa barabara zetu zimepakana sana na maeneo yenye huduma muhimu za wananchi kama vile afya, elimu, masoko, maduka na mikahawa, ambayo lazima mtu asimame na chombo, aegeshe ili azifikie.

166. MHESHIMIWA MASOUD AMOUR MASOUD (Jimbo la Amani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali kwa maboresho makubwa kwenye *entry points* zetu, hasa bandarini na uwanja wa ndege.

(a) Je, Serikali imejipangaje kwenye upande wa watumishi wa makampuni yanayotoa huduma kwenye maeneo hayo, ili watoe huduma zinazoendana na miundombinu hiyo.

(b) Je, ni kwa kiasi gani huduma bora za kiwango cha juu zinatolewa katika sehemu za Wageni Mashuhuri (VIP), zilizopo katika bandari na viwanja vyetu vya ndege.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

158. MHESHIMIWA MOZA MOHAMMED KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imechukua juhudi kubwa ya kupambana na utokomezaji wa kunguru ambapo fedha nyingi zimetumika kwa ununuzi wa mitego ya kunguru, badala ya fedha hizo kutumika katika mpango wa kuwasaidia wakulima kununua mbegu za kisasa za kuwasaidia kuimarisha kilimo cha kisasa na ufugaji wa mifugo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ng’ombe wa maziwa, mbuzi na kuku ambao utapunguza njaa kwa wananchi.

Kwanini Wizara imejielekeza katika kutumia fedha nyingi kutokomeza kunguru badala ya kutumia fedha hizo katika mpango wa kuwasaidia wakulima.

**<u>Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:</u>**

261. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kumeendelea kuongezeka kwa huduma ya uungwaji wa *Internet* inayotolewa na makampuni tofauti kwa kuwaungia wananchi kwenye maeneo yao wanayoishi (majumbani mwao).

Je, Serikali ina mashirikiano gani na kampuni zinazotoa huduma hiyo ya *internet* kwenye nyumba za wananchi.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

212. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Katika harakati za kujitafutia riziki, wananchi wa Pemba katika maeneo ya Mwambe, Vitongoji na Micheweni, wamekuwa wakibanja mawe ya kokoto kwa kutumia nyenzo duni kama vyuma na nyundo, vifaa ambavyo sio salama katika kazi zao hizo.

Je, Serikali itawasaidia vipi katika kuwapatia vifaa vya kisasa kama vile mashine maalumu za kukatia mawe ya kokoto, ili waendeleze kazi zao za kujipatia kipato.

**Wizara ya Afya:**

239. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (CHW - *Community Health Workers*) Mkoa Kusini Pemba, waliosomeshwa na kupatiwa simu kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa elimu ya afya kwa wananchi, hadi sasa hawajapatiwa simu hizo zilizochukuliwa awali kwa marekebisho, hali inayopelekea wapewaji huduma hiyo hawafikiwi ipasavyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wahudumu hao wanapatiwa simu hizo, ili waweze kufikisha huduma na elimu ya afya kwa wananchi kwa ufanisi

243. MHESHIMIWA MASOUD AMOUR MASOUD (Jimbo la Amani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali kwa kusambaza huduma za afya ndani ya Mji wa Zanzibar, ikijumuisha huduma za maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza.

(a) Ni sababu zipi zinazopelekea kuhamisha Kitengo cha kichocho kutoka hospitali ya Lumumba hadi hospitali ya Kivunge.

(b) Ni upi mpango wa Serikali wa kukirudisha Kitengo cha Kichocho katikati ya Mji wa Zanzibar kama ilivyo katika hospitali ya Kidongo Chekundu au Hospitali ya Sebleni, ili kurahisisha utoaji wa huduma wa kitengo hicho.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Taarifa ya Serikali Kuhusiana na Hali ya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2025.

Zanzibar,
17 Septemba, 2026.

(Ramadhan Khamis Juma)
KAIMU KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR